

Recent Kiswahili Books from Kenya – Nov 2022

Mary Martin Booksellers Pte Ltd
Blk 231, Bain Street
#03-05, Bras Basah Complex
Singapore 180231
Tel : +65-6883-2284/6883-2204
info@marymartin.com
www.marymartin.com

Literature

Mwongozo wa Bembea ya Maisha (Tamthilia) / John W. Wanjala
Nairobi: Teknobyte Publishers Limited, 2022
xxv, 55p.
9789914960020
\$ 15.00 / PB
106gm.

Madhumuni ya kuandika kitabu hiki ni kumrahisishia mwalimu na mwanafunzi kazi na kumpa mwelekeo unaofaa. Kitabu hiki kimeangazia masuala ibuka katika utahini wa karatasi ya tatu ya Kiswahili katika mtihani wa KCSE. Kitabu hiki kimejumuisha vipengele saba vya uhakiki wa fasihi andishi kama vile; Ploti ya tamthilia, dhamira ya mwandishi, mandhari na umuhimu wake, ufaafu wa anwani, maudhui, wahusika na uhusika na mbinu za lugha.

Maswali ya udurusu pia yamejumuisha katika kila mwisho wa onyesho ambayo yatamsaidia mwanafunzi kujinoa na kujipima ratili uelewa wake wa ploti. Maswali ya kiwango cha kitaifa pia yamejumuisha pamoja na majibu yake.

Masuala ibuka kama vile umuhimu wa wahusika, mbinu za kimtindo, aina za takriri, aina za taswira, na vipengele vingine.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835577>

Mwongozo wa Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine/ Shehe Mutwiri
Kenya: African Ink Publishers, 2022
120p.
\$ 25.00 / PB
164gm.

Waswahili husema cha mwenzako kikinyolewa chako tia maji. Kanseli imebadili mitindo ya utahini nasi sharti tubadili namna ya kuwaelekeza watahiniwa ili chombo kisiende mrama. Maswali ya karne ya 21 yanadhihirisha utahini wa stadi za umahiri na umilisi wa kazi ya fasihi na si kuiga tu kikasuku.

Mitihani ya kitaifa siku hizi inaegemea maswali yanayohitaji uwazaji wa kina, umilisi wa fasihi, usanisi au mbinu telekezi katika nadharia ya Bloom. Maswali ya kale ya maudhui na wasifu wa wahusika hayajitokezi kwa wingi kwani mtihani unalenga ufahamu mpana wa vitushi na msuko na si ufahamu wa kijuu juu tu.

Nakala hii ni mwongozo adhimu na aula kwa mwanafunzi na mwalimu wa shule ya upili kwani inaweka parauwanja maswala mbalimbali kama vile; Umuhimu wa ploti, umuhimu wa mandhari, umuhimu wa usimulizi, mtindo na mwingiliano matini wa vipengele mbalimbali. Nasadiki na kuamini mambo yatatengemea baada ya kupata nakala hii kwani kinolewacho hupata.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835578>

Najivunia Kuwa Mnandi / Ishamel Rono Nicodemus
Kenya: African Ink Publishers, 2021

Special Edition
v, 107p.
9789914995985
\$ 20.00 / PB
160gm.

Baada ya kuchinjwa, matumbo hukaguliwa na iwapo hakuna ishara yoyote ya ugonjwa, sherehe hutangazwa kuwa njema. Iwapo kondoo atapatikana na ishara ya ugonjwa, hii ikiwa nadra kwa kuwa umakinifu uliwekwa unapochaguliwa, mwingine hutakaswa na kuchinjwa tena. Rafiki zake bwana harusi wanapopeana habari njema, wazazi na wale kina mama wa ubatizo hunyunyiza maziwa na pombe...

<http://www.marymartin.com/web?pid=835579>

Wasya Wa Syokimau / David G. Maillu
Nairobi: African Comb Books Lts, 2019
182p.
9789966130860
\$ 25.00/ PB
204gm.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835580>

Kivuli cha Sakawa / Enlock Bitugi Matundura
Kenya: Nsemia Inc. Publishers, 2010
110p.
9781926906003
\$ 25.00 / PB
86gm.

Kivuli cha Sakawa (Sakawa's Ghost) , written in Kiswahili, the major lingua franca in the East African region, is a story about one of Africa's legendary heroes who was at the forefront in the battle against colonialism and its evils. Legend has it that he was a seer and that many of his predictions have come to pass.

In this this story, Sakawa finds himself at crossroads following the death of his father, a prominent leader in his own right. Conservative elders in his community who feel threatened by this youngster destined to be a great leader fight him tooth and nail to subdue his shining star. Will they succeed?

Sakawa Ng'iti indeed existed and lived among the Abagusii community in western Kenya at the turn of 19th Century (1800). The unfolding episode in this book did indeed take place, although probably in slightly a different way. By chronicling this episode, the author gives the story a new lease of artistic life and offers opportunity for others to comments and/or offer versions of the story as they understand it.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835581>

Kengeza La Jasiri / Shisia Wasilwa
Kenya: African Ink Publishers, 2022
vi, 228p.
9789914999181
\$ 20.00 / PB
234gm.

Jasiri ana Kengeza. Kengeza hilo halimpi amani. Linamsumbua maishani. Hilo kengeza linayaunganisha maisha yake ya zamani na usasa. Kalipata ujanani. Amekataa kulizika katika

kaburi la sahu. Je, Jasiri atapata tiba ya kengeza hilo analopenda, kulificha pembeni mwa kijoyo chake? Anagundua pia marehemu babake kaaga dunia kutokana na hilo kengeza. Je, haya makengeza ndiyo nini? Ni masimulizi yanayonata, yaliyosheheni taharuki na maudhui mazito.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835582>

Pandashuka (Riwaya) / Timothy Omusikoyo Sumba (Eds) Hamisi Babusa & Ken Walibora
Kenya: African Ink Publishers, 2022

vi, 180p.

9798582447788

\$ 18.00 / PB

192gm.

“Nikumbukapo mashaka tipitipi yaliyoizonga familia yetu naamini kuwa ulimwengu umefurika malimwengu ya kila nui ambayo hukingama mbele ya walimwengu maishani na kusababisha pandashuka. Kama barabara ndefu ilivyo safari ya Maisha haikosi mabonde, vilima, milima, tambarare na kona. Je. Ni gurufu gani isiyokuwa na gurufu? Kwa bahati njema mawimbi ya safari ngumu hayadumu maishani, huisha namna Maisha yenyewe yanavyoisha. Baadhi ya Pandashuka ni furaha na huzuni, raha karaha, vicheko na vilio, utajiri na umaskini, shibe na njaa, amani na vita, afya njema na maradhi, upendo na chuki n ahata shwari na shari namna wasemavyo wengine. Kimsingi, pandashuka hutusambazia ama utulivu au uchungu nzima unaozaa jakomoyo sufufu. Je, ni nani asiyejua kuwa painamapo ndipo painukapo?”

<http://www.marymartin.com/web?pid=835583>

Dau Lazama / Kulei G. Serem

Kenya: African Ink Publishers, 2021

x, 116p.

9798731585408

\$ 18.00 / PB

134gm.

Dau Lazama inatoa picha halisi ya mambo yanayoendelea katika jamii hususan katika bara la Afrika. Walalahoi katika taifa la Ngomeni wanapitia madhila yasiyo na kifani kutoka kwa walio na mamlaka ya dola. Ni bayana kwamba uongozi katika taifa hili ni wa kiimla. Tembo anatomia mbinu kali kuwakaandamiza wapinzani wa sera zake. Vilevile pana asasi muhimu za jamii kama vile dini, zinazofaa kuyanyosha maadili katika jamii ila sivyo katika taifa la Ngomeni: Mchungaji Kombo anauunga mkono ukoloni mamboleo na kushirikiana nao. Si hayo tu, siri kubwa inayozingira maisha ya kijana Bahati kuihusu usuli na hatima yake ya maisha inateka bakunja nadhari ya msomaji.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835584>

Adhabu Ya Maisha / Elishaphan Wachira

Kenya: African Ink Publishers, 2022

Special Edition

iv, 116p.

9789914996760

\$ 15.00 / PB

128gm.

Mwaisambe alipata taarifa kwamba katika jimbo lao la Matusitisi kulikuwako na mganga mashuhuri. Mganga huyo aliwatibu watu kwa dawa za kienyeji alizokuwa nazo daima. Basi baada ya kusikia habari kumhusu mganga huyo, Mwaisambe aliamua kwenda kumtembelea.

Ndugu Mwaisambe anaonekana kuishi maisha ya kubahatisha. Ni mfano wa vijana wanaoonekana kukosa ruwaza, wanabebwa hobelahobela na upepo wa nakama na kuwaangamiza. Mwaisambe yu safarini kumtafuta mganga mashuhuri asiyemjua asili wala fasili yake. Anapanda milima na kuivuka miamba hadi katika eneo la Kivunja Kimya. Atafaulu kumpata mganga wake? Jisomee upate kujua...

<http://www.marymartin.com/web?pid=835585>

Ndoa Ya Patashika (Riwaya) / David Ochola (Ed) Timothy Omusikoyo Sumba
Kenya: African Ink Publishers, 2021
vi, 204p.
9798725383362
\$ 20.00 / PB
214gm.

Ni mzazi kindakindaki. Ameniondolea janaa ya kuitwa mwana msi baba. Sasa nayafurahia mazingira matulivu. Yote ni kwa neema. Ile ndoa ya patashika baina ya Patashika na mama ikanitoka kabisa. Nikawa nimepoa na kutulia katika...
Ndoa ya Patashika ni riwaya inayoangazia masuala tata yanayojitokeza katika ndoa. Aghalabu, kila ndoa huwa na changamoto zayo na ndiye maana mwandishi ameyaweka tashtiti mambo yanayowaudhi wahusika katika ndoa zenye hali hizo.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835586>

Bembe ya Maisha / Timothy M. Arege
Nairobi: Access Publishers Limited, 2022
iv, 76p.
9789966194534
\$ 18.00 / PB
74gm.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835587>

Politics

Mikondo Ya Kiswahili : Siasa, Jamii na Utandawazi / Alamin Mazrui & Kimani Njogu
Nairobi: Twaweza Communications Ltd, 2022
xvi, 192p.
Includes Index
9789966128072
\$ 25.00 / PB
236gm.

The book, *Mikondo ya Kiswahili: Siasa, Jamii na Utandawazi (Trajectories in Swahili: Politics, Society, and Globalization)* is an exploration of trends--within the context of politics, society and globalization - of this most widely spoken African language. It is divided into two parts. Part I examines linguistic choices about the language - including translation and standardization--and the effects these have had in society. The colonial language hierarchies which minimized the status of Swahili vis-à-vis English, the authors argue undermined its pace of growth as a language of intellectual pursuits and constitutionalism. This first part of the book also discusses emerging variants of the language in Kenya. Part II discusses how Swahili is playing out within the East African Community as a lingua franca and as a key language of Pan-Africanism with its endorsement as a Working Language of the African Union. The book also revisits the arguments by historian Kumi Attobrah about *Afrihili* - an African language he created by incorporating the

grammar and lexical items from African languages. The last Chapter delves into the presence of Swahili in the United States of America and how it intersects with the Black Power Movement, the Cold War, and African Studies. The book has annexes of key position statements including *The Asmara Declaration on African Languages and Literatures of 2000*, which has now been made available in Swahili.

<http://www.marymartin.com/web?pid=835588>
